

**MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI APRILI, 2022 NA MWELEKEO
KWA MWEZI MEI, 2022.**

Dondoo za tathmini ya Aprili, 2022 na mwelekeo wa Mei, 2022:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Aprili, 2022 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2022 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Aprili 2022, maeneo mengi ya nchi yalipata vipindi vya mvua. Hata hivyo, vipindi vya ukavu vilijitokeza katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2022 hususan kwa maeneo ya kanda ya kati, nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya Kaskazini.
- Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua kubwa vimeripotiwa katika baadhi ya maeneo nchini.
- Mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2022 unaonyesha kuendelea kwa vipindi vya mvua katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.
- Ongezeko kidogo la joto linatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani.

1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2022.

Katika kipindi cha mwezi Aprili 2022, maeneo mengi ya nchi yalipata vipindi vya mvua. Hata hivyo, vipindi vya ukavu vilijitokeza katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2022 hususan kwa maeneo ya kanda ya kati, nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya Kaskazini. Kwa upande mwingine, vipindi vya mvua kubwa vimeripotiwa katika baadhi ya maeneo ya pwani ya Kaskazini, ukanda wa ziwa Victoria, maeneo

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

machache ya nyanda juu kaskazini mashariki, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi. Kiwango cha juu cha mvua cha milimita 137 kilipimwa katika kituo cha hali ya hewa kilimo cha Ukiriguru kilichopo Mwanza mnamo tarehe 27 Aprili, 2022. Aidha, kituo cha Matangatuani kilichopo kisiwani Pemba kilipima milimita 50.5 (tarehe 16 Aprili), 76.2 (tarehe 19 Aprili), milimita 93.2 (tarehe 20 Aprili) na milimita 62.5 (tarehe 28 Aprili, 2022). Maeneo mengine yaliyopima viwango vikubwa vya mvua ni pamoja na Zanzibar milimita 88.1 mnamo tarehe 15 Aprili, Pemba 86.3 (tarehe 20 Aprili), Bukoba 79.9 (25 Aprili), kituo cha Lyamungu kilichopo mkoani Kilimanjaro milimita 76.9 (tarehe 15 Aprili), Mbozi kilichopo mkoani Mbeya milimita 54.3 (tarehe 8 Aprili) na milimita 73.0 (tarehe 26 Aprili), Mahenge milimita 52.6 (tarehe 10 Aprili), Kizimbani kilichopo kisiwani Unguja milimita 50.6 (tarehe 26 Aprili), Songea milimita 57.1 (tarehe 26 Aprili) na Kibaha milimita 50.5 (tarehe 22 Aprili, 2022). Kwa upande mwingine, hali ya joto iliongezeka kidogo katika wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Aprili, 2022 kwa baadhi ya maeneo yaliyokuwa na upungufu wa mvua hususan nyanda za juu kaskazini mashariki

2.0 MWELEKEO KWA MWEZI MEI, 2022

2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2022 hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi na wastani hadi juu kidogo ya wastani katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola, hali ya joto la bahari la chini ya wastani inatarajiwa kuendelea. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi. Aidha, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini inatarajiwa kuimarika kidogo na hivyo kusababisha Ukandamvua kuendelea kusogea kuelekea kaskazini mwa nchi.

2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2022

Mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2022 unaonyesha kuendelea kwa vipindi vya mvua katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2022 ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia cha mwezi. Kwa upande mwingine, hali ya joto inatarajiwa kuongezeka kidogo katika baadhi ya maeneo ya nyanda za juu Kaskazini mashariki na ukanda wa Pwani. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2022 ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia cha mwezi.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika wiki ya kwanza ya mwezi Mei, 2022 ikifuatiwa na vipindi virefu vya ukavu katika kipindi kilichosalia cha mwezi Mei, 2022.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea kwa maeneo machache katika kipindi cha mwezi Mei, 2022.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea kwa maeneo machache katika kipindi cha mwezi Mei, 2022.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):

Vipindi vya ukavu vinatarajiwa kuendelea kwa maeneo mengi katika kipindi cha mwezi Mei, 2022.

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):

Vipindi vya ukavu vinatarajiwa kuendelea kwa maeneo mengi katika kipindi cha mwezi Mei, 2022. Aidha, vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa hususan katika sehemu za miinuko.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo machache hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2022.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):

Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache hususan wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Mei, 2022.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JUNI, 2022.

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2022, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache ya ukanda wa Pwani. Aidha, hali ya baridi inatarajiwa kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi.

2.4 USHAURI

Mvua za Masika zinaendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendeleo kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

Imetolewa tarehe 01 Mei, 2022 na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

727B -00/2019